# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU

*Dar es Salaam*
*31 Mei, 2025*

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa mafanikio yaliyopatikana nchini katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita yanatokana na utekelezwaji wa matakwa ya maendeleo na ustawi ya wananchi wa Tanzania kama yalivyoainishwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo mara baada ya kupokea Tuzo Maalum ya Heshima aliyotunukiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwa ni ishara ya kutambua uongozi wake mahiri uliolenga kuleta maendeleo jumuishi na ustawi wa Taifa.

Akielezea shukrani zake kufuatia kupokea Tuzo hiyo, Rais Dkt. Samia amesema kwake tuzo hiyo ni ishara ya kuthamini kazi ya pamoja kati ya mihimili ya dola, viongozi wa Serikali na wananchi wote kwa ujumla waliotoa ushirikiano wa karibu katika kipindi cha uongozi wa Awamu ya Sita na kuwezesha nchi kupata maendeleo.

Rais Dkt. Samia pia amelipongeza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa dhamira yake ya dhati ya kuisimamia Serikali kupitia mijadala ya bajeti, kwa kupitisha sheria muhimu, pamoja na kutoa ushauri kwa Serikali ambao umeongeza tija katika utendaji kazi katika ngazi zote.

Aidha, Rais Dkt. Samia amepongeza namna ambavyo Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Mungano wa Tanzania wanavyoendelea kuwasemea na kutetea maslahi ya wananchi wanaowawakilisha ndani na nje ya Bunge.

Kwa upande wake Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Tulia Ackson amempongeza Rais Dkt. Samia kwa uongozi wake wa kipekee na kueleza kuwa

Tuzo hiyo imetolewa kwa niaba ya Wabunge wote nchini kama ishara ya kutambua uongozi huo.

Hali kadhalika, ameeleza kuwa kupitia uongozi wa Rais Samia, Taifa limeshuhudia mageuzi makubwa katika kuimarisha Muungano, utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati, sambamba na maendeleo makubwa kwenye sekta za elimu, afya, madini, utalii, uchukuzi, kilimo, nishati na diplomasia ya kimataifa.

Spika Tulia pia amesema kuwa falsafa ya R4 (Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga Upya) imekuwa dira ya msingi ya Serikali ya Awamu ya Sita, ikionesha mwelekeo thabiti wa kulijenga Taifa lenye umoja, ustahimilivu na maendeleo jumuishi.

Shaaban Kissu
Naibu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu